TANGAZO LA SERIKALI Na. 23 la Tarehe 17/1/2025

SHERIA YA RELI,
(SURA YA 170)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 95(2)(n))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MATUMIZI YA MIUNDOMBINU YA RELI KWA WATOA HUDUMA BINAFSI ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 213 la 2024

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Matumizi ya Miundombinu ya Reli kwa Watoa Huduma Binafsi za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Matumizi ya Miundombinu ya Reli kwa Watoa Huduma Binafsi za Mwaka 2024 ambazo katika Kanuni hizi zitarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

**2**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 6(2) kwa-

(a) kufuta aya ya (d);

(b) kubadili mpangilio wa aya za (e) hadi (r) kuwa aya za (d) hadi (q) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 8

**3.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 8 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kanuni mpya ifuatayo:

"(3) Mmiliki wa leseni anayekusudia kuhuisha leseni atawasilisha maombi ya kuhuisha leseni kwa Mdhibiti ndani ya siku tisini kabla ya tarehe ya kuisha kwa muda wa leseni.".

Marekebisho ya kanuni ya 11
TS. Na.

**4**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 11(5) kwa kuongeza maneno "kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko za

26 la 2024

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini" mara baada ya neno "Mdhibiti".

Marekebisho ya kanuni ya 44

**5.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 44, kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (2); na
(b) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (3) kuwa kanuni ndogo ya (2).

Marekebisho ya Jedwali la Pili

**6**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Sehemu B ya Jedwali la Pili kwa kuongeza neno "SAFARI NDEFU ZA" kabla ya neno "ABIRIA" lililopo katika mstari wa pili wa safu ya kwanza.

Dodoma,
7th January, 2025

MAKAME M. MBARAWA,
*Waziri wa Uchukuzi*